WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS

WHI

TAASISI YA WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS

# TAARIFA YA MWAKA YA MFUKO WA UWEKEZAJI WA FAIDA (FAIDA FUND)




FAIDA FUND

*"Haba na Haba..."*

## KWA MWAKA UNAOISHIA 30 JUNI 2023

WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS

# TAASISI YA UWEKEZAJI WATUMISHI HOUSING

# TAARIFA YA MWAKA YA
# MFUKO WA UWEKEZAJI WA FAIDA (FAIDA FUND)




FAIDA FUND
*"Haba na Haba..."*

## KWA MWAKA UNAOISHIA
## 30 JUNI 2023

# YALIYOMO

1. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi ........................................................................................1
2. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko.......................................................................................4
3. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko .........................................................................6
4. Taarifa ya Hesabu za Mfuko ..............................................................................................9
5. Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji...............................................................................14
6. Taarifa ya Muda ya Mfuko wa Faida (Interim Report).......................................................21
7. Taarifa ya Muda ya Mfuko wa Faida (Interim Report).......................................................23

# WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS (WHI)

**MKUTANO MKUU WA KWANZA WA WAWEKEZAJI WA MFUKO WA FAIDA (FAIDA FUND)**

**SIKU YA JUMAMOSI, TAREHE 10 AUGUSTI 2024**
**KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE – DAR ES SALAAM**

**RATIBA NA AJENDA ZA MKUTANO**

| MTIRIRIKO WA SHUGHULI | | | |
|---|---|---|---|
| **NA** | **MUDA** | **SHUGHULI** | **WAHUSIKA** |
| 1 | 02.30 - 03.40 | Kuwasili kwa Wajumbe na Kujiorodhesha | Wajumbe/Utawala |
| 2 | 03.40 - 03.50 | Matangazo na Shughuli za Utawala | MC/Utawala |
| 3 | 03.50 - 04.00 | Kuthibitisha Akidi na Kufungua Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |
| 4 | 04.00 - 04.15 | Utambulisho (Wajumbe wa Bodi, Menejimenti, Wadau Waalikwa na Watoa Huduma wa Mfuko) | Mkurugenzi Mtendaji |
| 5 | 04.15 - 04.30 | Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi | Mwenyekiti wa Bodi |
| 6 | 04.30 - 05.15 | **Kupokelewa kwa Taarifa ya Mwaka:** | |
| | | Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko | Benki ya CRDB |
| | | Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu | CAG (PAMAK) |
| | | Taarifa ya Hesabu za Mfuko | Mkurugenzi wa Fedha |
| | | Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji | Mkurugenzi Mtendaji |
| 7 | 05.15 - 06.00 | Kipindi cha Maswali na Majibu | Mwenyekiti/ Watendaji |
| 8 | 06.00 - 06.15 | **Azimio la Mkutano Mkuu** na Kufunga Mkutano | Mwenyekiti wa Bodi |

FAIDA FUND "Haba na Haba..."

# TAARIFA YA MWAKA MFUKO WA FAIDA

# 1. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi

# TAARIFA YA MWENYEKITI



**Ndugu Wawekezaji,**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninayo furaha kuwakaribisha nyote katika Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Mfuko wa Faida (Faida Fund). Tunawashukuru kwa kutenga muda wa kuhudhuria mkutano huu ambao utajadili maendeleo ya Mfuko kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2023.

Ndugu wawekezaji, ninaamini mmekuwa mkifuatilia maendeleo ya Mfuko wa Faida na kwamba mmeipokea na kuisoma taarifa ya Mfuko kwa kipindi cha miezi nane kinachoishia tarehe 30 Juni 2023. Ninayo furaha kuwajulisha kuwa utendaji wa Mfuko kwa kipindi hicho ulikuwa mzuri. Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kigezo linganifu (Performance Benchmark). Faida kwa kipindi cha miezi nane (8) ya mwanzo kilichoishia 20 Juni 2023 ilikuwa asilimia 10.0 na imeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 12 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Faida iliyopatikana iko sawa na maendeleo ya soko la fedha na ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 9.7.

Katika kipindi hicho kilichoishia Juni 2023, thamani halisi ya mfuko iliongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 15.6 (Juni 2024 thamani ya Mfuko imefikia Shilingi bilioni 25.6). Ongezeko hili la thamani ya Mfuko linatokana na faida nzuri inayopatikana, matumizi ya tekinolojia katika kufanya miamala ya uwekezaji, kuongezeka kwa imani na elimu juu ya faida zinazopatikana kupitia Mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

Ongezeko la ukubwa wa Mifuko pia umetokana na ongezeko la idadi ya wawekezaji. Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2023 idadi ilifikia wawekezaji 2,041, hadi Juni 2024 idadi ilifikia wawekezaji 4,806 sawa na ongezeko la asilimia 58 la wawekezaji waliojiunga katika Mifuko.

**Mazingira katika Masoko ya Fedha**

Ndugu wawekezaji,

Maendeleo ya Soko la Mitaji na Dhamana, ambalo utendaji wake hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya Fahirisi (Tanzania Share Index), imeonesha kuwa na maendeleo mazuri. Katika kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni 2023, kumekuwa na ongezeko la asilimia 4.1 ambapo iliongezeka toka 3,928.5 tarehe 30 Juni 2022 hadi 4,091.8 tarehe 30 Juni 2023. Ongezeko hilo ni chini ya lile la tarehe 30 Juni 2022 ambalo lilikuwa ni asilimia 7.5. Hii inamaanisha kuwa, kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2023, bei za Hisa kwa ujumla ziliongezeka japo kwa kiwango kidogo ikilingwanishwa na mwaka uliopita.


Tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kusimamia na kuweka mazingira bora ya biashara.

**Matarajio**

Ndugu Wawekezaji, kwa kipindi kilichoishia Juni 2023, WHI imekuwa na mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Faida ambao unatoa pato shindani katika soko. Katika siku zijazo, WHI itaendelea kutekeleza mipango yake ikiwemo kuboresha mifuko na huduma kwa wawekezaji pamoja na kubainisha fursa nyingine za kibiashara kwa manufaa ya wawekezaji, Serikali pamoja na wadau wengine. WHI itaendelea kuboresha mfumo wa uendeshaji wa mifuko ili uwe wa kisasa zaidi na kuhakikisha wawekezaji wanapata faida shindani na nzuri kuendana na hali ya soko.

**Shukrani**

Ndugu Wawekezaji, Katika kuhitimisha taarifa yangu, napenda niwashukuru nyote kwa ushirikiano na imani yenu kwa WHI na Mfuko wa Faida kwa kipindi chote kilichoishia tarehe 30 Juni 2023. Kwa namna ya kipekee nipende kuishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Msimamizi wa Mifuko ambaye ni Benki ya CRDB, Soko la Hisa la Dar es Salaam pamoja na Madalali wake, Wajumbe wenzangu wa Bodi ya Wakurugenzi, Wafanyakazi wa WHI na Wadau wote ambao wameendelea kuiwezesha WHI kutekeleza majukumu yake. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utaendelea kwa manufaa ya Wawekezaji wetu na maendeleo ya Soko la Mitaji na Sekta ya Fedha hapa Nchini kwetu.



Abdul-Razaq Badru

**Mwenyekiti wa Bodi**

# 2. Taarifa ya Mwangalizi wa Mfuko

**CRDB BANK PLC**
Makao Makuu:
Barabara ya Ally Hassan Mwinyi / Barack Obama
S.L.P. 268, Dar es Salaam – Tanzania
Simu: +255 (0) 22 211 7441-7
Nukushi: +255 (0) 22 211 6714
Barua pepe: info@crdbbank.co.tz
Tovuti: www.crdbbank.co.tz

# TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO WA FAIDA KWA WAWEKEZAJI

Tukiwa ni waangalizi wa Mfuko wa Faida, Jukumu letu ni kusimamia kwamba utendaji wa Meneja wa Mfuko unaendana/ unazingatia waraka wa makubaliano ili kuhakikisha maslahi bora ya wenye vipande. Katika utekelezaji wa kazi hii, Mwangalizi wa Mfuko ana majukumu yafuatayo:

a) uangalizi wa mali za mfuko;

b) kuhakikisha meneja wa mfuko anatumia njia/mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya mfuko sambamba na mkataba wa makubaliano; na pia

c) kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa.

Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, kilichoanzia Mfuko ulipoanza mauzo ya awali ya vipande tarehe 01.11.2022 mpaka 30.06.2023, Benki ya CRDB kama Mwangalizi wa **Mfuko wa Faida**, tumeendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za Meneja wa Mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

Kwa kuzingatia hayo, tunapenda kuwathibitishia kwamba shughuli za uwekezaji kwenye **Mfuko wa Faida** na wajibu wa Meneja wa Mfuko (Watumishi Housing Investments), vimetekelezwa kufuatana na vipengele vya Waraka wa Makubaliano. Tukizingatia suala la imani/ uaminifu wa wenye vipande kwenye mfuko, tunathibitisha kwamba maslahi ya wenye vipande ndani ya **Mfuko wa Faida** yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo, na meneja ameendesha mfuko kulingana na Waraka wa Makubaliano.

*Abdulmajid M. Nsekela*
**Afisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji**

Tarehe: **31 Julai, 2024**

# 3. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko

**Controller and Auditor General,**
National Audit Office, Audit House,
4 Ukaguzi Road,
P.O. Box 950,
41101 Tambukareli,
Dodoma, Tanzania.

Tel: 255 (026) 2161200
Fax: 255 (026) 2117527
E-mail: ocag@nao.go.tz
Website: www.nao.go.tz

# TAARIFA YA MKAGUZI KUHUSU MUHTASARI WA HESABU ZA MFUKO WA FAIDA

**Maoni**

Muhtasari wa hesabu za Mfuko ambao unajumuisha muhtasari wa Urari wa Hesabu za Mfuko mnamo tarehe 30 Juni 2023, muhtasari wa Mapato na Matumizi, muhtasari wa Mabadiliko ya Thamani ya Mfuko pamoja na muhtasari wa Mtiririko wa Fedha umetayarishwa kutoka katika taarifa kamili ya ukaguzi ya Mfuko wa Faida kwa kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2023.

Kwa Maoni yetu, Muhtasari wa Hesabu za Mfuko wa Faida unaendana na taarifa kamili za hesabu za Mfuko zilizokaguliwa kulingana na vigezo vilivyoelezwa kwenye Dokezo Namba 1.

**Muhtasari wa Taarifa ya Hesabu za Fedha**

Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha haioneshi taarifa zote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (IFRS standards as issued by the International Accounting Standards Board (IFRS standards)). Muhtasari huu wa hesabu pamoja na hii taarifa yetu siyo mbadala wa taarifa kamili ya hesabu za kifedha iliyokaguliwa. Muhtasari wa hesabu za kifedha pamoja na taarifa kamili ya hesabu zilizokaguliwa haijumuishi matukio au miamala baada ya tarehe za taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

**Taarifa ya Ukaguzi na Hesabu za Fedha zilizokaguliwa**

Maoni ya ukaguzi (audit opinion) yasiyokuwa na kasoro juu ya taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha za Mfuko yalitolewa kwenye taarifa ya tarehe 20 Machi 2024 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Taarifa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023 inajumuisha mambo mengine muhimu juu ya ukaguzi wa hesabu za mfuko.

**Majukumu ya Meneja Kuhusu Muhtasari wa Hesabu za Fedha za Mfuko**

Meneja wa Mfuko anahusika na utayarishwaji wa muhtasari wa hesabu za fedha za Mfuko kwa mujibu wa vigezo kama ilivyoainishwa kwenye Dokezo Namba 1.

**Majukumu ya Mkaguzi wa Hesabu za Mfuko**

Majukumu yetu kama wakaguzi wa hesabu za Mfuko ni kutoa maoni kama muhtasari wa Hesabu za Mfuko unaendana na taarifa kamili ya ukaguzi wa hesabu za fedha na kwa mujibu wa taratibu zetu za ukaguzi, ukaguzi ambao ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi (International Standars on Auditing-ISA) 810 (kama ilivyorekebishwa), “Kazi za kuripoti juu ya Muhtasari wa taarifa za kifedha”

**Hili ni toleo lililotafsiriwa la ripoti ya Mkaguzi iliyosainiwa katika toleo la Kiingereza.**

**Dokezo Namba 1**

**Dokezo juu ya vigezo vya kutayarisha Muhtasari wa Hesabu**

Muhtasari wa taarifa ya hesabu za fedha umetayarishwa kutoka kwenye taarifa kamili ya ukaguzi, iliyotayarishwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha (IFRS standards)

mnamo tarehe 30 Juni 2023.

Taratibu za kutayarisha muhtasari wa hesabu za fedha unaitaka menejimenti kuamua kiwango cha taarifa zitakazojumuishwa katika muhtasari ili kuendana kwa kiwango kikubwa na taarifa kamili ya ukaguzi au kutoa taswira ya muhtasari iliyosawa na taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa.

Menejiment imetayarisha hesabu hizi kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

a) Muhtasari wa Hesabu unajumuisha hesabu zote za mfuko zilizoko katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa;
b) Taarifa zilizopo kwenye muhtasari wa hesabu zinashabihiana na taarifa ya hesabu za mfuko zilizokaguliwa; na
c) Jumla kuu, jumla ndogo pamoja na taarifa linganifu zilizopo kwenye hesabu zilizokaguliwa zimeonyeshwa pia katika muhtasari wa hesabu ulioandaliwa.

Taarifa ya hesabu za mfuko wa Faida zilizokaguliwa zinapatikana katika ofisi ya Taasisi ya Nyumba na Uwekezaji (Watumishi Housing Investments).

# 4. Taarifa ya Hesabu za Mfuko

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

*(Statement of Income or Loss and Other Comprehensive Income)*

## KWA KIPINDI CHA MIEZI NANE KINACHOISHIA 30 JUNE 2023

| | Miezi Nane Hadi 30 Juni 2023 |
|---|---|
| | TSH'000 |
| **MAPATO** | |
| Mapato yatokanayo na Riba | **1,021,094** |
| **Jumla ya Mapato** | **1,021,094** |
| | |
| **MATUMIZI** | |
| Gharama za Meneja | **(112,244)** |
| Gharama za Mwangalizi wa Mfuko | **(6,926)** |
| Gharama za Mauzo ya Vipande | **(1,228)** |
| Gharama Nyinginezo za Uendeshaji | **(40,953)** |
| **Jumla ya Gharama za Uendeshaji** | **(161,352)** |
| | |
| **Ongezeko la Thamani kwa Wenye Vipande kabla ya Kodi** | **859,743** |
| | |
| Kodi ya Zuio | **(3,219)** |
| **Mapato halisi baada ya Kodi** | **856,523** |
| Mapato Mengineyo | **-** |
| **Ongezeko Halisi la Thamani ya Mfuko** | **856,523** |

# URARI WA HESABU ZA MFUKO

*(Statement of Financial Position)*

## MNAMO TAREHE 30 JUNI 2023

| | 2023 |
|---|---|
| | **TSH'000** |
| **RASILIMALI ZA MFUKO** | |
| Fedha Taslimu | 1,000,759 |
| Amana katika Mabenki | 545,210 |
| Dhamana za Serikali | 14,340,117 |
| Dhamana za Makampuni | 100,000 |
| Rasilimali Nyinginezo Ambazo Hazijalipwa | 192,454 |
| **Jumla ya Rasilimali** | **16,178,540** |
| | |
| **DHIMA YA MFUKO** | |
| Dhima Nyinginezo | **(632,921)** |
| **Jumla ya Dhima ya Mfuko** | **(632,921)** |
| | |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **15,545,619** |
| | |
| **Inawakilishwa na:** | |
| Mtaji wa Vipande | **14,689,095** |
| Ongezeko Halisi la Thamani ya Mfuko | **856,524** |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **15,545,619** |
| | |
| Thamani ya Kipande | **104.9707** |

# TAARIFA YA MABADILIKO YA THAMANI YA MFUKO

*(Statement of Net Assets Attributable to Unitholders)*

## KWA KIPINDI CHA MIEZI NANE KINACHOISHIA 30 JUNE 2023

| | 2023 |
|---|---|
| | TSH'000 |
| Thamani ya Mfuko Julai 1 | - |
| Mabadiliko/Ongezeko la Mfuko | 856,524 |
| | **856,524** |
| **Miamala ya Wenye Vipande kwa Mwaka** | |
| Mauzo ya Vipande | 14,866,871 |
| Ununuzi wa Vipande | (177,776) |
| **Mabadiliko ya thamani ya Mfuko** | **14,689,095** |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **15,545,619** |

FAIDA FUND
"Haba na Haba..."

# TAARIFA YA MTIRIRIKO WA MAPATO

*(Cash Flow Statement)*

## KWA KIPINDI CHA MIEZI NANE KINACHOISHIA 30 JUNE 2023

| | 2023<br>TSH'000 |
|---|---:|
| **Fedha Itokanayo na Shaghuli za Uendeshaji** | |
| Mapato yaliyopokelewa kwenye uwekezaji wa dhamana za serikali | 739,456 |
| Mapato yaliyopokelewa kwenye uwekezaji wa taasisi za kifedha | 5,235 |
| Kodi ya Zuio iliyolipwa | (3,219) |
| **Fedha halisi iliyotumika kwenye shughuli za uendeshaji (A)** | **741,472** |
| | |
| **Shughuli za Uwekezaji** | |
| | |
| Fedha zilizotumika kwenye uwekezaji katika taasisi za kifedha | (545,210) |
| Amana katika Mfuko wa Ukwasi | (389,167) |
| Ununuzi wa dhamana za serikali | (13,880,755) |
| Ununuzi wa dhamana za Makampuni | (100,000) |
| **Fedha halisi iliyotumika kwenye shughuli za uwekezaji (B)** | **(14,915,132)** |
| | |
| **Amana ya Mfuko** | |
| | |
| Mauzo ya vipande (Sale of units) | 14,866,871 |
| Ununuzi wa vipande (repurchase of units) | (177,776) |
| **Fedha halisi iliyotokana na miamala ya wenye vipande (C )** | **14,689,095** |
| | |
| Ongezeko Halisi la Fedha (A+B+C) | 515,437 |
| Salio la amana katika Mfuko wa Ukwasi | 485,322 |
| Salio la fedha mwanzoni mwa mwaka | - |
| **Salio la fedha mwisho mwa mwaka** | **1,000,759** |

..........................................
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Tarehe:** Agosti 2024

..........................................
**Mwenyekiti wa Bodi**
**Tarehe:** Agosti 2024

# 5. Taarifa ya Meneja Kuhusu Uwekezaji

# TAARIFA YA MENEJA KUHUSU UWEKEZAJI



## 1. Kuanzishwa kwa Mfuko


Mfuko wa Faida ulianzishwa mwezi Novemba 2022 na kuanza rasmi mauzo ya vipande tarehe 1 Januari 2023. Ni mfuko wa uwekezaji wa pamoja ambao hutoa fursa kwa Taasisi na watu binafsi kuwekeza kipato chao cha ziada kwa kipindi kifupi cha kati au muda mrefu kwa faida na ukwasi madhubuti.

Mahitaji ya awali ya uwekezaji ni shilingi elfu kumi (Tsh 10,000) na kiwango cha nyongeza sio chini ya shilingi elfu tano (Tsh 5,000). Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza. Mwekezaji anaruhusiwa kuchukua fedha zake wakati wowote baada ya kumalizika siku tisini (90) tangu alipowekeza mara ya kwanza. Malipo hufanyika ndani ya siku tatu (3) za kazi bila kutozwa gharama ya kutolea (exit load), hivyo kudhihirisha Mfuko wa Faida ni fursa maridhawa kwa wawekezaji.

## 2. Thamani Halisi ya Mfuko


Hadi tarehe 30 Juni 2023 thamani halisi ya Mfuko ulifikia shilingi bilioni 15.55. thamani ya kipande ilifikia Tsh 104.9707 kutoka Tsh 100.0000 kwa kipande tarehe 1 Januari 2023. Ukuaji wa thamani halisi ya Mfuko unaonyeshwa katika Chati Namba 1.

**Chati Na 1: Thamani Halisi ya Mfuko wa Faida hadi tarehe 30 Juni 2023**




Kulingana na taarifa ya muda ya kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2024 Mfuko wa Faida umeendelea kukua na kufikia thamani halisi ya Shilingi bilioni 25.96 kutoka Shilingi bilioni 15.35 sawa na ongezeko la asilimia 41. Hali kadhalika thamani halisi ya kipande iliongezeka kufikia Shilingi 115.8120 kwa kipande tarehe 30 Juni 2024 kutoka thamani Shilingi 104.9707 kwa kipande kwa taarifa ya tarehe 30 Juni 2023.

**Chati Na 2: Ukuwaji wa Mfuko wa Faida (Juni 2023 Mpaka Juni 2024)**





| | Jun-23 | Sep-23 | Dec-23 | Mar-24 | Jun-24 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukubwa wa Mfuko (TZS'000) | 15,350 | 16,302 | 19,242 | 21,119 | 25,499 |
| Thamani Halisi ya Kipande | 104.9707 | 107.6086 | 110.2360 | 112.9776 | 115.8120 |

## 3. Mgawanyo wa Uwekezaji

Mgawanyo wa uwekezaji ulizingatia sera ya uwekezaji ya Mfuko wa Faida. WHI kama Meneja wa Mfuko alitumia uzoefu na weledi katika kufikia mgawanyo anuai wa rasilimali ili kupata mapato makubwa bila kuathiri ukwasi wa Mfuko. Kwa kipindi cha miezi nane kinachoishia tarehe 30 Juni 2023, mgawanyo wa uwekezaji wa Mfuko ni kama inavyoonekana kwenye Chati Namba 3 hapa chini.

**Chati Na 3: Mgawanyo wa Uwekezaji Mpaka Juni 2023**



Mgawanyo wa uwekezaji katika Mfuko wa Faida katika Chati Namba 3 inaonesha Mfuko umewekeza zaidi kwenye dhamana za muda mrefu kwa kiasi cha asilimia 91 (serikali asilimia 90 na makampuni asilimia 1), asilimia 3 kwenye amana za benki za muda maalumu na asilimia 6 iliwekezwa kwenye amana za benki za muda mfupi. Aidha, uwekezaji katika amana za muda mfupi umefanywa ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa mfuko ikiwemo kulipa fedha kwa wawekezaji pindi wanapouza vipande vyao.

### 4. Faida kwa Wawekezaji

Faida kwa wawekezaji ilikuwa kubwa ikilinganishwa na kigezo linganifu (Performance Benchmark). Faida kwa kipindi cha meizi nane (8) ya mwanzo kilichoishia 20 Juni 2023 ilikuwa asilimia 10.0 na imeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 12 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Faida iliyopatikana iko sawa na maendeleo ya soko la fedha na ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 9.7 (Dhamana ya Serikali ya Miaka 5).

Mambo mengine ya kuzingatia katika kulinganisha faida za uwekezaji katika Mfuko wa Faida na amana za mabenki:

a) Mapato yatokanayo na uwekezaji katika Mfuko wa Faida haitozwi kodi ya zuio (withholding tax) wakati viwango vya riba za mabenki ni kabla ya kutoa kodi ya suio.

b) Mfuko wa Faida unaruhusu wawekezaji wake kuuza vipande vyao wakati wowote (baada ya kumalizika kipindi cha siku 90 tangu mwekezaji alipowekeza mara ya kwanza) hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata fedha pindi anapozihitaji.

c) Hakuna gharama wakati wa kuingia (kuwekeza) na kutoka (kuuza vipande) katika Mfuko.

d) Aina nyingine ya uwekezaji katika masoko ya fedha zina muda maalum wa ukomo wake, uwekezaji katika Mfuko wa Faida hauna muda maalum wala ukomo.

e) Mwekezaji anaweza kutumia vipande alivyowekeza Mfuko wa Faida kama dhamana ya kupata mkopo benki.

f) Aidha Mfuko unatoa suluhisho la uwekezaji kwa makundi maalumu kama vile wastaafu, Watoto, wawekezaji wa Pamoja (joint investors) n.k.

Kwa ujumla kuwekeza kwenye Mfuko wa Faida kuna faida zaidi ya kuwa na akaunti ya amana kwa sababu inamuongezea mwekezaji kipato kikubwa kutokana na viwango bora vya faida vinavyotolewa na mfuko na fursa nyingine nyingi.


### 5. Mwenendo wa Uchumi Tanzania

#### 5.1 Pato la Taifa na Mfumuko wa Bei

Kigezo cha Pato Halisi la Taifa kwa mwaka 2023 kinaonyesha uchumi ulikua kwa kiwango cha asilimia 5.1, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 4.7 mwaka 2022 (kama ilivyooneshwa kwenye Chati Namba 4). Ukuaji wa uchumi mwaka huu 2024 unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.6 kutokana na jitihada za serikali zinazoendelea katika kukuza na kutekeleza miradi ya kimkakati hasa katika sekta za, Kilimo, Ujenzi, usafirishaji na Madini. Ukuaji unachagizwa na kufufuliwa kwa shughuli za kiuchumi hususani uwekezaji kwenye sekta ya umma na binafsi nchini.

Aidha mfumuko wa bei umeendelea kushuka kutoka asilimia 4.4 mwaka 2022 hadi asilimia 4 mwaka 2023 na unatarajiwa kushuka hadi takribani asilimia 3.1 mwaka huu 2024 kama Chati Na.4 inavyoonesha.

**Chati Na 4: Mwenendo wa Ukuwaji wa Uchumi na Mfumuko wa Bei**




*Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)*


Pato la taifa hutafasiri kiwango na shughuli za uchumi katika nchi. Hali imara na stahimilivu juu ya mwenendo wa uchumi nchini ni muhimu kwa Mifuko ya uwekezaji wa pamoja inayosimamiwa na WHI na maeneo mengine ya uwekezaji nchini. Uchumi imara husaidia kutunza na kuimarisha thamani ya uwekezaji na huvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

### 5.2 Sekta ya Benki

Kwa kipindi cha mwaka mmoja ulioishia tarehe 30 Juni 2023, hali ya utendaji kwa sekta ya benki nchini imeendelea kuwa stahimilivu na yenye faida. Mifumo ya malipo kwa njia ya kidigitali nchini iliendelea kuwa imara, ikithibitishwa na kuwepo kwa kiwango cha juu cha miamala iliokamilika kwa muda mfupi. Aidha, kuwepo kwa mifumo imara na thabiti kumehamasisha Umma kuendelea kuamini na kutumia mifumo kwenye huduma mbalimbali za kifedha.

Jumla ya rasilimali ziliongezeka na kufikia shilingi trilioni 53.7 mwezi Juni 2023 kutoka shilingi trilioni 46.16 iliyonakiliwa Juni 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16.3. hali kadhalika kiasi cha amana kiliongezeka na kufikia shilingi trilioni 33.7 kutoka shilingi trilioni 32.6 iliyonakiliwa Juni 2022 sawa na asilimia 3.3. Jumla ya mikopo iliyotolewa na mabenki ilifikia ilishilingi trilioni 31.5 Juni 2023 kutoka shilingi trilioni 26.1 Juni 2022. Mwenendo wa ukuaji katika sekta ya benki unaonyeshwa katika Chati Namba 5.

**Chati Na 5: Mwenendo wa Ukuaji Secta ya Benki**




*Chanzo: Repoti ya Sekta ya Benki Tanzania – Chapisho la Uchambuzi 2024*

Ongezeko hilo linatokana na imani ya Umma katika secta ya benki, mazingiza mazuri ya kiuchumi na mikakati mizuri ya kuhamasisha amana inayotekelezwa na mabenki na taasisi za fedha nchini.

Kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki ni muhimu kwa uchumi na mifuko ya uwekezaji wa pamoja na kwa ujumla ukiwemo Mfuko wa Faida. Meneja wa Mfuko amefanikiwa kuunganisha mifumo ya WHI na Mfumo wa Malipo Serikalini (GePG) na benki ili kuwawezesha wawekezaji kununua vipande kidigitali, hivyo kurahisisha uwekezaji mahali popote. Wawekezaji pia wanaweza kufanya malipo ya uwekezaji mtandaoni popote Duniani kupitia kadi za kimataifa za *Visa, MasterCard* na *American Express*.

### 5.3 Soko la Mitaji na Dhamana

Kwa kipindi hadi Juni 2023 soko la mitaji na dhamana limekuwa imara na thabiti, kwani limepelekea kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji katika soko la hisa, mitaji, dhamana na kwenye Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja. Katika kipindi hicho, mbali na kuanzishwa kwa Mfuko wa Faida uliovutia wawekezaji na kunakili jumla ya shilingi bilioni 7.9 mwezi Decemba 2022, tulishuhudia utoaji wa hatifungani mbili mpya za benki ya taifa ya biashara (NBC - Twiga) na benki ya biashara ya Kenya (KCB - Fursa Sukuk) zilizofanikiwa kufanya vizuri kwani jumla ya shilingi bilioni 49.9 zilipatikana.


Hali ya ushiriki kwenye soko la mitaji na dhamana nchini imeongezeka na moja ya sababu kubwa ni kutokana na umma kupata uelewa kuhusu uwekezaji na matumizi ya mifumo ya kidigitali. Ni matarajio yetu kuwa hali hii itazidi kuimarika na kuongezeka zaidi. Kuingia kwa Wasimamizi wapya wa Mifuko (Meneja wa Mifuko) ya uwekezaji wa pamoja na dhamana mpya sokoni ni ishara nzuri kwa WHI na soko kwa ujumla. Tunatarajia Taasisi au kampuni zingine kujiunga ili kuongeza ukwasi na ushindani sokoni jambo ambalo litaongeza zaidi ufanisi, faida na huduma bora kwa wawekezaji.

### 5.4 Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni

Viwango vya kubadilisha fedha kati ya Shilingi ya kitanzania na fedha za kigeni vimeendelea kuwa stahimilivu nchini. Thamani ya Shilingi kwa Dola moja ya kimarekani ilikuwa imara na ya kuridhisha ikisaidiwa na kuwepo kwa hali nzuri kwenye bei za bidhaa na huduma nchini. Takwimu zinaonyesha kuwa thamani ya fedha nchini imebaki kuwa imara, ingawa, ilipungua thamani dhidi ya Dola ya Marekani

kwa asilimia 1.0 (Tsh 23.4) hadi Tsh. 2,339.1 mwaka 2023 kutoka Tsh. 2,315.7 iliyorekodiwa mwaka uliopita. Mwenendo unaonyeshwa katika Chati Namba 6 hapa chini.

**Chati Na 6: Mwenendo wa Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni**




*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

Ustahimilivu wa viwango vya kubadilisha fedha ni muhimu kwa mifuko ya uwekezaji wa pamoja na Uchumi wa Tanzania kwa ujumla kwani husaidia kutunza thamani ya rasilimali ambazo thamani yake ipo katika shilingi za kitanzania. Kwa ujumla, Mifuko inayosimamiwa na WHI inatoa faida nzuri kwa Shilingi za Tanzania lakini inapobadilishwa hadi sarafu nyingine kama vile Shilingi Dola ya Marekani faida inaweza kuathiriwa endapo kutakuwa na kupungua kwa thamani ya shilingi ya kitanzania katika kipindi hicho.

### 5.5 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, taasisi za usimamizi wa mifuko ya uwekekezaji wa pamoja nchini zinahusisha taasisi kuu mbili ambazo ni; Taasisi ya UTT Asset Management and Investor Services (UTT AMIS), pamoja na Taasisi ya Watumishi Housing Investments (WHI). Hivi karibuni mwezi Mei 2024 taasisi ya Zan Securities imeingia sokoni kama meneja wa mfuko. Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, jumla ya rasilimali kwenye mifuko inayosimamiwa na Taasisi hizo ni shilingi bilioni 1,610.67 kama ifuatavyo:

a) Mifuko ya uwekezaji inayosimamiwa na UTT AMIS kwa ujumla ilikuwa na rasilimali zipatazo Shilingi bilioni 1,535.4.

b) Mifuko ya uwekezaji inayosimamiwa na WHI kwa ujumla ilikuwa na rasilimali zipatazo Shilingi bilioni 85.27 (Mfuko wa WH-REIT Shiling bilioni 69.27 na Mfuko wa Faida Shilingi bilioni 15.55).

***Vyanzo:** Taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu, CMSA, UTT AMIS, Banki Kuu ya Tanzania.*

# 6. Azimio la Mkutano Mkuu

Azimio la Mkutano Mkuu wa Wawekezaji wa Mfuko wa Faida **unaazimia kuipokea na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Mfuko wa Faida ikiwemo Taarifa ya Hesabu za Mfuko wa Faida kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2023.**

FAIDA FUND
"Haba na Haba..."

# 7. Taarifa ya Muda ya Mfuko wa Faida (Interim Report)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS

# TAARIFA YA MUDA YA BODI YA WAKURUGENZI YA WATUMISHI HOUSING INVESTMENTS KWA KIPINDI KILICHOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024

MFUKO WA FAIDA – (FAIDA FUND)

FAIDA FUND

"Haba na Haba..."

Imechapishwa na Kuwasilishwa CMSA

Julai 2024

# TAARIFA YA MUDA YA BODI YA WAKURUGENZI WA MFUKO WA FAIDA KWA KIPINDI KILICHOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024

1. **Utangulizi**

   Bodi ya Wakurugenzi ya Watumishi Housing Investments (WHI) inawasilisha taarifa ya muda ya Mfuko wa Faida kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2024. Mfuko ulianza mauzo ya vipande ya awali tarehe 01 Novemba 2022 na kunakili faida ya Shilingi milioni 658.56 kwa hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2023.

2. **Uanzishwaji na Usimaizi wa Mfuko**

   Mfuko wa Faida ni mfuko wa uwekezaji wa pamoja ulioanzishwa na WHI, ambayo ni Taasisi ya Umma chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR MUUUB) ilianzishwa tarehe 06 Februari 2013 chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212. Mfuko wa Faida ulianzishwa chini ya Hati ya Dhamana (*Trust Deed*) ya Mfuko wa Faida na unasimamiwa na Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja) za mwaka 1997, zilizowekwa chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, 1994.

   Mfuko unasimamiwa na WHI, Meneja wa Mfuko aliyesajiliwa ambaye ameweka muundo wa usimamizi ili kutekeleza shughuli za kila siku za Mfuko. Majukumu ya Meneja wa Mfuko yameainishwa katika Kifungu cha 4.0 cha Waraka wa Toleo.

   Mwangalizi wa Mfuko ni benki ya CRDB, ambayo ni benki ya biashara iliyopewa leseni ya kufanya biashara ya benki chini ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, 2006. Majukumu ya Mwangalizi wa Mfuko yameainishwa katika Kifungu cha 5.5 cha Waraka wa Toleo.

3. **Majukumu na Malengo ya Mfuko**

   Jukumu la mfuko ni kuwekeza fedha zilizokusanywa katika mgawanyo sahihi utakaowawezesha wawekezaji wa kipato cha juu na cha chini kupata mapato shindani katika muda wa kati na mrefu kupitia ukuwaji wa mtaji.

   Malengo makuu ya Mfuko ni:

   a) Ukuaji wa Mitaji: Mfuko unawapa Watanzania fursa ya kushiriki katika soko la mitaji na kupata faida nzuri kutokana na uwekezaji wao.

   b) Kukuza Utamaduni wa Kuweka Akiba: Mfuko kwa kuwa ni bidhaa ya kifedha ya gharama nafuu, unawawezesha Watanzania kupitia umiliki mpana wa vipande vyake, huhimiza utamaduni wa kuweka akiba katika rasilimali za kifedha.

4. **Mauzo na Ununuzi wa Vipande vya Mfuko**

   Bei ya mauzo na ununuzi wa vipande inategemea Thamani Halisi ya Kipande iliyopo tarehe ya mauzo au ununuzi bila gharama za kuingia au kutoka, mtawaliwa.

5. **Matumizi ya Fedha za Uwekezaji**

   Fedha za uwekezaji zinawekezwa katika vyombo vya masoko ya fedha na mitaji.

6. **Tahadhari**

   Uwekezaji katika mifuko ya pamoja unapaswa kuzingatiwa kama uwekezaji wa muda wa kati hadi mrefu. Wawekezaji wanapaswa kutambua kwamba uwekezaji katika Mfuko unakabiliwa na hatari za soko na Thamani Halisi ya Mfuko (NAV) inaweza kupanda au kushuka kulingana na sababu na nguvu zinazoathiri soko la dhamana. Utendaji wa awali si lazima uhakikishe utendaji wa siku zijazo.

7. **Uwezo wa Kulipa Madeni na Ukwasi**

Urari wa Hesabu za Mfuko mnamo tarehe 30 Juni 2024 inaonyesha kuwa Mfuko unaweza kutimiza majukumu yake ya muda mrefu ya kifedha. Pia Sera ya Uwekezaji ya Mfuko inahakikisha upatikanaji wa ukwasi wa kutosha huku ikitoa mapato ya ushindani kwa wawekezaji. Hivyo, Meneja wa Mfuko anauchukulia Mfuko kuwa wenye uwezo wa kutimiza majukumu yake.

8. **Bodi ya Wakurugenzi**

Maelezo ya Wakurugenzi walioshika madaraka katika kipindi cha nusu mwaka na hadi tarehe ya taarifa hii ni kama ifuatavyo:

| Na | Jina | Umri | Nafasi | Tarehe ya Uteuzi | Hali / Tarehe ya Ukomo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mr. Abdul-Razaq Badru | 56 | Mwenyekiti | 06 February 2024 | Yupo |
| 2 | CPA Hosea Kashimba | 53 | Mwenyekiti | December 2018 | 06 Februari 2024 |
| 3 | Bw. Bernard Konga | 43 | Mjumbe | 1 July 2016 | Yupo |
| 4 | Bw. Masha J. Mshomba | 53 | Mjumbe | 4 April 2021 | Yupo |
| 5 | Bw. Hamad Abdallah | 52 | Mjumbe | 24 February 2023 | Yupo |
| 6 | Bw. Shabani S. Mande | 50 | Mjumbe r | 30 August 2021 | Yupo |
| 7 | Dkt. Fred Msemwa | 51 | Mkurugenzi Mtendaji na Katibu wa Bodi | 1 November 2013 | Yupo |

Wakurugenzi wote ni Wanzanian. Taarifa hii pia inapatikana katika tofuti: www.whi.go.tz.

*Imesainiwa*

.................................................

Dkt Fred Msemwa
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Tarehe:** 31 Julai 2024

# MFUKO WA FAIDA (FAIDA FUND)

Taarifa ya hali ya kifedha ya Mfuko wa Faida kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2024. Ilichapishwa kwa mujibu wa Sehemu ya XIII, Kifungu cha 38(1) cha Kanuni za Masoko ya Mitaji na Dhamana (Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja), 1997.

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**

**KWA KIPINDI KILICHOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024**

| | Kipindi Kilichoishia 30 Juni 2024<br>TSH'000 | Kipindi Kilichoishia 30 Juni 2023<br>TSH'000 |
|---|---|---|
| Mapato yatokanayo na Riba | **2,487,481** | **850,411** |
| Mapato Mengineyo | **-** | **-** |
| **Jumla ya Mapato** | **2,487,481** | **850,411** |
| Gharama za Uendeshaji | (365,712) | (188,634) |
| **Ongezeko la Thamani kwa Wenye Vipande kabla ya Kodi** | **2,121,769** | **661,777** |
| Kodi ya Zuio | **(8,204)** | **(3,219)** |
| **Ongezeko la Thamani kwa Wenye Vipande Baada ya Kodi** | **2,113,566** | **658,558** |
| Mapato Mengineyo | **-** | **-** |
| **Ongezeko la Thamani kwa Wenye Vipande Baada ya Kodi** | **2,113,566** | **658,558** |

# MFUKO WA FAIDA (FAIDA FUND)

**URARI WA HESABU ZA MFUKO**
**MNAMO TAREHE 30 JUNI 2024**

| | 30-Juni-24 | 30-Juni-23 |
|---|---|---|
| | TSH'000 | TSH'000 |
| **RASILIMALI ZA MFUKO** | | |
| Fedha Taslimu | 1,399,308 | 1,000,759 |
| Amana katika Mabenki | 745,210 | 545,210 |
| Dhamana za Serikali | 23,537,922 | 14,145,380 |
| Dhamana za Makampuni | 200,000 | 100,000 |
| Rasilimali Nyinginezo Ambazo Hazijalipwa | 586,878 | 189,226 |
| **Jumla ya Rasilimali** | **26,469,318** | **15,980,575** |
| | | |
| **DHIMA YA MFUKO** | | |
| Dhima Nyinginezo | **(509,330)** | (632,920) |
| **Jumla ya Dhima ya Mfuko** | **(509,330)** | **(632,920)** |
| | | |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **25,959,987** | **15,347,654** |
| | | |
| **Inawakilishwa na:** | | |
| Mtaji wa Vipande | **22,989,790** | 14,689,096 |
| Ongezeko la Thamani Lililobakia | 856,632 | - |
| Ongezeko la Thamani kwa Wenye Vipande | **2,113,566** | 658,558 |
| **Thamani Halisi ya Mfuko** | **25,959,987** | **15,347,654** |
| | | |
| Thamani Halisi ya Kipande kwa Vipande Vilivyouzwa Hadi Tarehe 30 Juni 2024 | **115.8120** | **104.9707** |

..................................................

Dkt Fred Msemwa
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Tarehe:** 31 Julai 2024



Watumishi Housing Investments (WHI)
6th Floor Golden Jubilee Towers, Ohio / Garden Street.
P.O Box 5119, Dar Es Salaam. Tanzania.
Tel: +255 22 2922211, Fax: +255 22 2922221
Email: info@whi.go.tz / wekeza@whi.go.tz, Website: www.whi.go.tz

@watumishihousinginvestments